# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

## KIKAO CHA SABA

**05 FEBRUARI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

## KIKAO CHA SABA – TAREHE 05 FEBRUARI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU:

**108. MHESHIMIWA LATIFA KHAMIS JUAKALI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatambua Vijana wenye ujuzi ambao hawatambuliki rasmi ili kuwaendeleza.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**109. MHESHIMIWA SILYVESTRY FRANCIS KOKA (KIBAHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, nini hatma ya Shirika la Elimu Kibaha.

**110. MHESHIMIWA DKT. CHARLES STEPHEN KIMEI (VUNJO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni Shule zipi chakavu katika Jimbo la Vunjo zimewekwa kwenye Mpango wa kufanyiwa ukarabati.

**111. MHESHIMIWA INNOCENT EDWARD KALOGERIS (MOROGORO KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Afya Kata ya Singisa na Bwakila Juu katika Jimbo la Morogoro Kusini.

**112. MHESHIMIWA VITA RASHID KAWAWA (NAMTUMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Kisasa cha Mabasi - Namtumbo.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**113. MHESHIMIWA NANCY HASSAN NYALUSI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Umma ili kuendana na kasi ya maendeleo na kuongeza ufanisi.

**114. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA KIKOYO (MULEBA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapa posho ya mazingira magumu Wafanyakazi hasa Walimu wanaopangiwa kazi Mikoa ya pembezoni.

**OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

**115. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, lini Serikali itawalipa Wastaafu waliokuwa Wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanaodai fomula haikufuatwa wakati wanalipwa.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**116. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali imefanya tathmini ya kujua ni miti mingapi inayopandwa inatunzwa na kukua ili kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi.

**WIZARA YA NISHATI:**

**117. MHESHIMIWA UMMY ALLY MWALIMU (TANGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwaunganishia umeme wa gharama nafuu Wananchi wa maeneo ya pembezoni yenye sifa za Vijiji - Tanga.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**118. MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILLA (ULYANKULU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuruhusu maeneo ya Hifadhi yaliyokosa sifa yatumike kwa matumizi ya kilimo na makazi.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**119. MHESHIMIWA TAMIMA HAJI ABASS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Kampeni ya Shujaa wa Maendeleo wa Ustawi wa Jamii Tanzania (SMAUJATA) imeleta matokeo gani tangu kuzinduliwa.

**WIZARA YA UJENZI:**

**120. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, kwa nini Serikali isiboreshe Barabara zote nchini kwa kuongeza Barabara za waenda kwa miguu na pikipiki.

121. **MHESHIMIWA JACQUELINE NGONYANI MSONGOZI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Wananchi wa Vijiji vya pembezoni mwa Barabara ya Lumecha – Londo – Mpepo Morogoro watalipwa fidia.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

122. **MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Baada ya Serikali kulipa fidia eneo la Liganga na Mchuchuma lini uwekezaji utaanza.

**WIZARA YA MAJI:**

123. **MHESHIMIWA CHARLES JOHN MWIJAGE (MULEBA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, nini mpango wa Serikali kutekeleza Miradi ya Maji katika Kata 5 za Ziwani, Kata za Muleba Magharibi na Gwanseli - Kagoma.

## WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

**124. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, fursa zipi zitapatikana kwa Mtanzania mmoja mmoja na vikundi kupitia Fainali za Mpira wa Miguu kwa Nchi za Afrika.

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**125. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, upi Mkakati wa Serikali kutoa elimu kwa Wananchi kuhusu umuhimu wa utoaji Chanjo dhidi ya Magonjwa ya Wanyama.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**126. MHESHIMIWA MINZA SIMON MJIKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kununua magari ya Zimamoto kwa ajili ya Wilaya za Mkoa wa Simiyu.

**127. MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY (MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Polisi Tarafa za Daudi na Nambis Wilayani Mbulu.

## IV. HOJA ZA KAMATI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**DODOMA**
**05 FEBRUARI, 2025**

**BARAKA I. LEONARD**
**KATIBU WA BUNGE**